

OR - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA



Phone: +255 768 941 492
E-Mail: maselass2006@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI MASELA
S.L.P. 255
MASWA.
01/12/2020

KUMB.Na.MSLSS/AD/J/F.I/VOL.I/01/2021/.....

KWA MZAZI / MLEZI WA:

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASELA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanao aliyetajwa hapo juu, amechaguliwa kujunga na Shule hii kidato cha kwanza kwa mwaka 2021. Ni matumaini yangu kuwa mwanao ataitumia nafasi hii **adimu** vizuri kwa **kusoma kwa bidii**, nidhamu na maarifa katika kuendeleza kipaji chake kwa muda wote atakaokuwa hapa shulenii.

Shule itafunguliwa kwa wote **siku ya Jumatatu tarehe 11/01/2021 asubuhi**. Siku hiyo ufile shulenii ukiwa na mwanao na mahitaji yote muhimu ya shule. Mwisho wa kuripoti ni **tarehe 22/01/2021**

2. TARATIBU NA HALI YA SHULE.

Shule hii ni mchanganyiko (wavulana na wasichana) Wanafunzi wote wanapaswa kuwa makini kwa kuzingatia na kufuata taratibu zote za shule. **Kupuuza na kukiuka taratibu za shule kwa makusudi** kutasababisha mwanafunzi kuachishwa masomo. Sheria za shule zimeambatanishwa, Hivyo zisome kwa makini na kuzielewa.

3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

3.1. Sare za shule

a. **Wavulana** - Suruali jazi mbili, kitambaa cha **rangi ya BLUE BAHARI** jazi moja na **rangi ya BLUE** jazi moja zenye marinda mawili na upana chini wa **nchi 16** mzunguko, shati nyeupe mikono mifupi jazi mbili, viatu vyeusi nya kufunika vyenye visigino vifupi na nya kufunga na kamba, soksi **NYEUEPE** jazi mbili kwa Wavulana.

b. **Wasichana** - sketi jazi mbili kitambaa cha **rangi ya BLUE BAHARI** (jazi moja) na **rangi ya BLUE** (jazi moja) mashono linda box kila moja urefu ufile kifundo cha mguu, mkanda wake (waist band) usizidi nchi 2 (zitakaguliwa shulenii) viatu vyeusi nya kufunika vyenye kisigino kifupi na nya kufunga na kamba, soksi **NYEUEPE** ndefu jazi mbili.

c. **Sweta la shule rangi ya BLUE kwa wasichana na wavulana**

d. **Sare ya michezo** (i) **T-shirt** rangi kijani kibichi (**rangi ya jeshi**) yenye nembo ya shule kwa wote (wavulana na wasichana). (ii) **Traki suit** ya rangi blue bahari kwa wasichana, kwa wavulana bukta rangi ya bluu. (iii) viatu nya raba vyeusi kwa wote wavulana na wasichana

3.2 MAHITAJI YA SHULE

Mwanafunzi atatakiwa kufika shulenii na mahitaji yafuatayo:

- Madaftari makubwa 10 (counter book)
- Vifaa kama rula, kalamu, mkebe
- Kamusi ya kiingereza (dictionary)

3.3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 20 ya mwaka 1978 inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini,. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi

yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika vipindi ndani na nje ya darasa ni muhimu.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara kufuga kucha ndefu, kufuga ndevu, kuvaav mavazi yasiyo na heshima, kupaka rangi ya kucha na midomo, kunyoa kipara, wala kupigana au kugombana.,
4. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaav sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na.
9. Kutunza mali ya umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia biashara ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- iv. Makosa mengine ya Jinai
- v. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au ya watu wengine.
- vii. Kudharau Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
- viii. Kuoa au kuolewa
- ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- x. Kutoa au kushawishi kutoa mimba
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- xii. Kukataa adhabu halali.
- xiii. Kujiachisha shule mwenyewe
- xiv. Kukataa kufanya mitihani au mazoezi ya masomo
- xv. Kuwa na simu ya mkononi.

NAAMBATANISHA NA FOMU ZIFUATAZO

- i. Medical Examination Form ambayo itatakiwa kujazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Pia fomu hii aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni.
- ii. Fomu ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa shuleni.

NB: Soma Kwa Makini Maelezo / Maagizo Haya Na Kuyatekeleza Kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MASELA
“*Nidhamu na Maarifa Daima*”.


EMMANUEL C. BULIUCI
MKUU WA SHULE

MASELA SECONDARY SCHOOL
HEADMASTER
MASELA SECONDARY SCHOOL

OR - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
SHULE YA SEKONDARI MASELA



Phone: +255 768 941 492
E-Mail: maselass2006@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI MASELA
S.L.P. 255
MASWA

MEDICAL EXAMINATION REQUEST FORM

Please examine the above mentioned girl/boy as to her/his fitness for studies in this school. (This form must be filed in by the Government medical officer).

Student's full name:.....

Present Age:.....

Blood test.....

Stool examination:.....

T. S. Test:.....

Asthma:.....

Eye disorder:.....

Norse disease:.....

Sickle cell Anaemia:.....

Chest:.....

Operations:.....

Serious accidents:.....

Pregnancy:.....

(in case of female)

ADDITIONAL INFORMATION E.g.: Physical defects or impairment, chronically family

Diseases etc:.....

I (Full name) have examined the above named
and consider that he/she is Physically **fit / unfit** for a full time schooling course.

Signature:..... Designation:.....

Date :..... Official stamp:.....

HEADMASTER
MASELWA SECONDARY SCHOOL
MASWA

OR - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
SHULE YA SEKONDARI MASELA



Phone: +255 68 941 492
E-Mail: maselass2006@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI MASELA
S.L.P. 255
MASWA.

**FOMU YA MAMBO BINAFSI NA MIKATABA YA MWANAFUNZI/MZAZI/MLEZI NA SHULE
(PERSONAL PARTICULARS).
(IJAZWE KWA HERUFI KUBWA)**

1. jina
kamili.....
.....
 2. tarehe ya
kuzaliwa.....mwezi:.....mwaka:.....
.....kabila.....
 3. uraia:.....
.....
 4. dini yakedhehebu
 5. (a) Anwani kamili ya nyumbani(yaani kwa wazazi/walezi)
.....
.....
(b) Wakati wote wa masomo taja mahali utakapokaa.....
5. (a) Jina la
mzazi/mlezi.....hai/amefariki
Anwani yake.....
Eneo analoishi.....(muhimu kuweka namba zinazopatikana)
Simu.....
- TAMKO LA MWANAFUNZI.**
6. (a) Mimi.....nina kiri na
kukubali kwamba kipindi chote cha masomo sitajihusisha na migomo/fujo/makosa ya jinai,
ikitokea sheria zichukuliwe mkondo wake.
.....sahih.....tarehe.....
Jina

TAMKO LA MZAZI/MLEZI.

- (b) Mimi.....mzazi/mlezi wa mwanafunzi huyu, nakubali
mtoto wangu asajiliwe katika Shule ya kutwa ya Masela Sekondari. Ninaahidi kutoa ushirikiano
wa karibu katika kumlea na kumwendeleza kitaaluma. Aidha nakubali kumwezesha kikamilifu
kwa kumpatia mahitaji yake muhimu ya shule ili aweze kutulia Shuleni na kuweka bidii katika
masomo yake.
Jinatarehe.....
sahih.....